JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

ANUANI: KEREZANGE SEKONDARI'
NAMBA YA SIMU: 0716 022526
BARUA PEPE kerezangesecschool@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI KEREZANGE
S.L.P 18169
DAR ES SALAAM

---

Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………..

YAH:MAELEKEZOYA KUJIUNGANA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULEYA SEKONDARI KEREZANGE MWAKA ........................

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga katika shule ya sekondari Kerezange mwaka ........... kidato cha tano katika Tahasusi ya ……………. Nakupongeza kuwa mmoja kati ya wanafunzi waliopata nafasi ya kujiunga na shule za sekondari za serikali.

Shule hii ipo mkoa wa Dar es salaam, katika Halmashauri ya jiji la Dar es salaam, kata ya kivule karibu na ofisi ya mtendaji wa kata ya Kivule, umbali wa mita 200 kutoka barabara kuu iendayo Kivule.
Shule hii ni ya kutwa na ni mchanganyiko wa wavulana na wasichana.
Muhula wa masomo utaanza mwezi Julai. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ________________. Mwisho wa kuripoti ni tarehe _____________

1. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE ZA SHULE

i. WASICHANA

a) Sketi mbili (2) rangi ya dark blue. Urefu wa sketi ni lazima uwe sm 15 chini ya magoti. Mshono wa sketi uwe wa V – SHAPE upande wa mbele. Kwa wanafunzi wa kiislam ni lazima sketi ifike kwenye kifundo cha miguu.
b) Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi. (Kwa wanafunzi wa kiislam wanaovaa Hijabu. Juba nyeupe mbili (2) ndefu zinazofunika kifua na zifikie kwenye kifundo cha mikono anaposimama. Nusu kanzu nyeupe mbili (2) ndefu zenye kusitiri).
c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba vyenye visigino vifupi.
d) Soksi nyeupe ndefu zisizo na urembo.
e) Tshirt mbili za rangi ya dark blue (zinapatikana shuleni)
f) Sweta rangi ya dark blue
g) Tai yenye mistari ya dark blue na nyeupe

h) Sare za michezo ni raba nyeupe na truck suit ya Tanzania rangi ya bluu yenye ufito wa njano.

ii. WAVULANA

a) Suruali mbili (2) za rangi ya dark blue zenye marinda mawili, zenye mifuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma. Ziwe na pindo chini na urefu zifike kwenye kisigino.
b) Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi.
c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba vyenye visigino vifupi.
d) Soksi nyeusi ndefu zisizo na urembo.
e) Tshirt mbili za rangi ya dark blue (zinapatikana shuleni)
f) Sweta rangi ya dark blue
g) Tai yenye mistari ya dark blue na nyeupe
h) Mkanda mweusi wa ngozi. Usiwe na urembo
i) Sare za michezo ni raba nyeupe na truck suit ya Tanzania rangi ya bluu yenye ufito wa njano.

B) MICHANGO MBALIMBALI

| S/N | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji wa shule | 35,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | JUMLA | 50,000/= |

NB. Malipo haya yalipwe kupitia bank ya CRDB, akaunti namba 0150251325500. Jina la akaunti ni KEREZANGE SECONDARY SCHOOL. Unapofanya malipo hakikisha umeandika jina la mwanafunzi. Mwanafunzi aje ya bank pay in slip siku ya kuripoti shuleni ikionyesha jina kamili la mwanafunzi, kidato na Tahasusi.

C) VIFAA VYA KUJIFUNZIA

1) Madaftari saba (7) counter book quire 4.
2) Begi jeusi la kubeba mgongoni lisilo na urembo
3) Ream mbili (A4) za karatasi nyeupe kwa mwaka.
4) Vitabu vya tahasusi husika
5) English dictionary na kamusi ya Kiswahili kwa wanaosoma somo la Kiswahili.

D) VIFAA VYA USAFI

1) HGL: Anatakiwa kuleta ndoo ndogo, fagio la ndani(soft broom), na fagio la nje
2) HKL: Anatakiwa kuleta ndoo ndogo, fyekeo na sabuni ya maji ya dukani lita 5.
3) HGK: Anatakiwa kuleta jembe lenye mpini na fagio la nje lenye mpini.

2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mijibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye jukumu na dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Ni lazima kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu.
3. Kuwahi shuleni na katika shughuli nyingine utakazopewa.
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote uwapo shuleni.
5. Kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule.
6. Kuvaa kikamilifu sare ya shule wakati wote unapotakiwa. Ivaliwe kwa heshima kama ilivyoelekezwa.
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ikiwa ni pamoja na kuingia darasani.
8. Ni muhimu kuzingatia utunzaji wa vifaa na mali za umma.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa mitindo au kufuga ndevu kwa wavulana. Nywele ziwe fupi.
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuweka dawa kwenye nywele au kupaka rangi/hina kwenye kucha za vidole/mikononi na mwilini.

3. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

a) Utoro wa kutokuja shule na utoro wa vipindi
b) Wizi
c) Kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi/uasherati/ushoga/ ubakaji/ulawiti.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, shisha na kadhalika.
e) Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzako, mwalimu au mfanyakazi yeyote.
f) Kudharau Bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa na wimbo wa shule.
g) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
h) Kukataa adhabu kwa makusudi.
i) Kuharibu mali za umma kwa makusudi.
j) Kupata ujamzito/kumpa mimba mwanafunzi mwenzako.
k) Kuoa au kuolewa.
l) Kutumia lugha za matusi
m) Kuchora au kuandika kwenye kuta, meza na viti.
n) Kukutwa au kutumia simu ya mkononi shuleni.
o) Kucheza kamali na michezo ya kubahatisha

4. UTARATIBU WA SHULE

a) Unatakiwa ufike shuleni kati ya saa 12:30 asubuhi hadi saa 1:00 asubuhi na kuondoka shuleni baada ya vipindi vyote kwa mujibu wa ratiba ya shule.
b) Ukifika shuleni ni lazima ushiriki kufanya usafi katika eneo ulilopangiwa.
c) Ni lazima kuwepo darasani vipindi vyote. Huruhusiwi kuwa nje ya shule/darasa wakati wa ratiba ya masomo.
d) Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
e) Huruhusiwi kupiga kelele wakati wote unapokuwa darasani na kwenya mazingira ya shule.
f) Utii wa kengele ya shule ni lazima kwani ndiyo itakayo kuelekeza juu ya unatakiwa uwepo wapi na unapaswa kufanya nini kwa wakati gani.
g) Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana kwenye vilabu vya pombe (bar, night clubs, vigodoro) kumbi za starehe, nyumba za kulala wageni (guest house, hotel and lodges)
h) Kwa kuzingatia umuhimu wa lishe bora kama yalivyo maelekezo ya serikali, wanafunzi wote watapata chakula cha mchana shuleni kwa gharama ya tshs 22,000/= kila mwezi. Fedha hiyo itapokelewa shuleni.

MUHIMU: Mwanafunzi na mzazi wanapaswa kusoma na kuelewa vizuri maelekezo yaliyoko katika fomu mbalimbali na kujaza vizuri na kuiwasilisha shuleni.

5. VIAMBATISHO VYA FOMU

a) Fomu Na 1, Fomu inayoeleza historia ya Mwanafunzi na mzazi/mlezi.
b) Fomu Na 2, Fomu ya mwanafunzi kuhusu Ahadi juu ya kutii na kufuata taratibu na sheria za shule.
c) Fomu Na 3, (Medical Examination form’) itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.

KARIBU SANA

_______________

MAGOMA ELIAKIMU MAGOTI
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KEREZANGE
FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI

Fomu Na 02
Picha ya mwanafunzi

(a) Ijazwe na mwanafunzi

1. Jina kamili la mwanafunzi …………………………………………………
2. Uraia ………………………………………………………………………..
3. Dini ………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………
5. Mkoa aliozaliwa ……………………………………………………………..
6. Yatima/aliyefiwa na mzazi mmoja/aliyefiwa na wazazi wote ……………………………
7. Kata unayoishi ………………………………………
8. Mtaa unaoishi ……………………………………….
9. Shule alizosoma kabla ya kujiunga na shule ya sekondari Kerezange

| JINA LA SHULE | KIDATO | MWAKA WA MASOMO |
|---|---|---|
| | | |
| | | |

Sahihi ya mwanafunzi: ……………………..................
Tarehe: ……………………

(b) Maelezo binafsi ya Mzazi /Mlezi

1. Jina kamili la Mzazi/ Mlezi ………………………………….……. Picha ya mzazi
2. Uraia……………………………………….………………..
3. Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi………………………….…………..
4. Sehemu unayoishi …………………………………….…………
5. Mtaa ……………………………………………………………
6. Namba ya nyumba ……………………………...…………
7. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi …………………………………
8. Sahihi ya mwenyekiti wa serikali ya Mtaa unapoishi……………………… muhuri……………….

Namba ya simu……………………………………..

(c). Uhusiano wako na mwanafunzi ………………………………………

(d). Kazi anayofanya mzazi/mlezi………………………....... Sahihi ya mzazi/mlezi…………………

Fomu Na 02

Picha ya Mwanafunzi

Mkuu wa Shule
Shule ya Sekondari Kerezange
S.L.P 18039
DAR ES SALAAM

YAH: AHADIYAMWANAFUNZI JUUYAKUTII NAKUFUATATARATIBU NASHERIA ZA SHULEKAMAZILIVYOELEKEZWA.

Mimi …………………..……………………………… (mwanafunzi husika) mwanafunzi wa kidato cha ……….............. Tahasusi ya …………… katika Shule ya Sekondari ya Kerezange.

Naahidi kuwa nipo tayari kufuata na kuheshimu sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelekezwa ili kuchochea maendeleo yangu ya shule na Taifa kwa ujumla.

Aidha naahidi kuwa endapo nitakwenda kinyume na ahadi hii hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu na hata ikibidi nifukuzwe shule.

Sahihi ya mwanafunzi ………………………….
Tarehe……………………..

Na ahidi mbele ya;

i. Mzazi/mlezi wangu, Jina……………………………………………………………………..

   Sahihi ya mzazi/mlezi…………………………. Namba ya simu……………………………

ii. Mwenyekiti wa serikali ya mtaa unaoishi, Jina………………………………………………

   Sahihi na mhuri……….……………. Namba ya simu ……………………

Fomu Na. 03

KIAMBATANISHO ‘B’
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA MINISTRY OF
EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING STUDENT
MEDICAL CERTIFICATE

(To be complete by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster/headmistress of Kerezange Secondary School P.O. BOX 18169 Dar es salaam.)

To the Medical Officer,
Date:…………………………..
……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

RE: ……………………………………………………………………………………………………
Please, examine the student mentioned above and comment on his/her health by responding to the following items. Kindly put a “tick” or “cross” in front of either.

3. Do the student have problems in connection with:-
(a) Sight? (1) No (2) Yes
(b) Hearing? (1) No (2) Yes
(c) Speech? (1) No (2) Yes
If yes, state ……………………………………………………………………………………….
(d) T.B? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………………
(e) Blood Pressure? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………………
(f) Any physical disability? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………………
(g) Asthma? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………………
(h) Sickle cell anaemia? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………………

4. Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this School?
(l) No (2) Yes, if no, please state reasons.
……………………………………………………………………………………………………………

Date:……………………………… Name & Signature of M.O……………………………..
Designation & Stamp ………………………………….